AGA KHAN MUSIC
AWARDS

# Washindi wa Tuzo za Muziki za Aga Khan 2022 watangazwa

## Washindi watambuliwa kwa kuzungumzia masuala ya sasa ya kijamii na mazingira huku wakidumisha na kuendeleza mapokeo ya kimuziki

**Geneva, Switzerland, Oktoba 6, 2022** –Washindi wa Tuzo za Muziki za Aga Khan 2022 (AKMA) watangazwa leo. Tuzo hizi za kila baada ya miaka mitatu, ambazo zilianzishwa na Mtukufu Aga Khan mwaka 2018, zinabaini ubunifu wa kipekee, kipaji na biashara katika muziki kwenye jamii mbalimbali diniani ambazo Waislamu wapo kwa wingi. Washindi wa tuzo hizi na watu waliopewa Shukrani Maalum watagawana fedha za zawadi $500,000 sambamba na fursa za kuendeleza taaluma zao. Fursa hizi zinahusisha kupewa kazi za kutunga nyimbo mpya, mikataba ya kurekodi na usimamizi wa wasanii, kuungwa mkono katika miradi ya elimu, na ushauri wa kiufundi au usimamiaji wa miradi ya uhifadhi, utunzaji na usambazaji wa muziki.

Tuzo za Muziki za Aga Khan zinaakisi imani ya Mtukufu Aga Khan, Imamu mrithi wa 49 wa Waislamu wa Ismaili, kwamba muziki unaweza kutumika kama nguzo ya utamaduni, ambayo inaimarisha hali ya mtu kujiona sehemu ya jumuiya, utambulisho na urithi, na wakati huo huo ukiwafikia kwa nama iliyo madhubuti watu wa tamaduni nyingine.

Wakati wa kutangaza washindi, Jopo la Majaji wa Tuzo hizi lilionesha shauku ya kuwaunga mkono wagombea wengi kadri iwezekanavyo kati ya wanamuziki 400 kutoka nchi na tamaduni mbalimbali iwapo kutatokea uhitaji wa haraka wa wanamuziki na waelimishaji wa muziki. Pamoja na kutoa mchango wao katika uhifadhi na udumishaji endelevu wa urithi wa muziki, washindi wengi miongoni mwao wanatumia nguvu ya muziki kukuza uelewa wa masuala ya kijamii na mazingira.

Washindi wa Tuzo za Muziki za Aga Khan watafanyiwa sherehe katika hafla na mfululizo wa matukio yanayohusika na hafla hii yatakayofanyika jijini Muscat, Falme za Oman, ambayo yameandaliwa kwa kushirikiana na Tuzo za Ujenzi za Aga Khan (AKAA), Oktoba 29-31, 2022.

**Washindi wa Tuzo za Muziki za Aga Khan 2022:**

<u>Washindi</u>

- **Zakir Hussain (India)**
  Tuzo Maalum ya Heshima kwa kutambua aina ya muziki wake iliyo maarufu sana na inayogusa utamaduni mtambuka iliyoinua hadhi ya *tabla* nchini India na ulimwenguni kote kupitia ushirikiano na wasanii wasio na idadi, ziara za matamasha, kazi za kutunga nyimbo mbalimbali, tungo zake na vibwagizo vya filamu.

- **Afel Bocoum (Mali)**
  Mwimbaji na mpiga gitaa kutoka Niafunké, Mali ambaye muziki wake unatumia mchanganyiko wa gitaa pamoja na ala mahalia za muziki ili kupata sauti ya “desert blues” kupitia mtindo wa muziki wa asili na jadi.

- **Asin Khan Langa (India)**
  Mpiga *sarangi*, muimbaji, mtunzi na mwanaharakati wa jumuiya ya muziki ya Langa ambayo ni urithi wa Rajasthan, na msanii wa mashairi ya Sufi yaliyopangiliwa katika mahadhi ya muziki wa jadi na kisasa.

- **Coumbane Mint Ely Warakane (Mauritania)**
  Mwimbaji na mpiga *ardin* (kinubi) kutoka Trarza, magharibi kusini mwa Mauritania, ambaye anaimba muziki wawnahekaya wa Mauritania kwa mtindo wa jadi hasa.

- **Daud Khan Sadozai (Afghanistan)**
  Kinara wa *Afghan rubab* ambaye amekuwa na mchango mkubwa katika uhifadhi, uendelezaji na usambazaji wa muziki wa watu wa Afghanistan duniani kote.

- **Peni Candra Rini (Indonesia)**
  Mtunzi, mboreshaji, muimbaji na muelemishaji wa Indonesia ambaye maarifa yake ya sanaa ya maonesho ya Indonesa husaidia katika uandaaji wa kazi mpya duniani kote.

- **Soumik Datta (UK)**
  Mpiga *sarod* anayechanganya ujuzi wake wa muziki wa asili wa Hindustani katika muziki wa *pop*, *rock*, *electronica* na vibwagizo vya filamu kukuza uelewa wa masuala muhimu ya kijamii ikiwemo mabadiliko ya tabia nchi, wakimbizi na afya ya akilia.

- **Yahya Hussein Abdallah (Tanzania)**
  Mwimbaji na mtunzi wa nyimbo za dini na msomaji wa Qur’an kutoka Dar es Salaam, Tanzania ambaye anatunga na kuimba kwa Kiswahili na baadhi ya lugha mahalia 126 za Tanzania.

- **Yasamin Shahhosseini (Iran)**
  Chipukizi mahiri wa *oud* ambaye analeta mageuzi ya matumizi ya ala hii ya muziki

katika muziki wa Iran kupitia tungo zake za kibunifu.

• **Zarsanga (Pakistan)**

Mwimbaji kutoka Khyber Pakhtunkhwa, Pakistan, anajulikana kama Malkia wa Ngano za Pashtun (*Queen of Pashtun Folklore*) kwa kujihusha kwa muda mrefu na shughuli za muziki wa asili unaoimbwa kupitia fasihi simulizi za makabila ya Pashtun.

Shukrani Maalum

• **Dilshad Khan (India)**

Mpiga *sarangi* wa kizazi cha kumi kutoka uzao wa Rajasthan ambaye anapanua lugha ya sarangi katika muziki wa filamu na kupitia tungo za kibunifu kwa kushirikiana na wasanii wengine kutoka tamaduni mbalimbali.

• **Golshan Ensemble (Iran)**

Hawa ni wanawake wanne ambao wanaimba muziki wa jadi wa Iran wenye mahadhi ya kisasa na wanafanya kazi kama walimu, kwa kuweka mkazo maalum katika kurithisha mapokeo ya muziki wao kwa wasichana na wanawake.

• **Sain Zahoor (Pakistan)**

Mwanamuziki wa Punjabi ambaye kwa muda mrefu amekuwa mwimbaji wa mashairi ya Sufi katika mahekalu na matamasha mahalia, mara nyingi ikiambatana na uchezaji densi kwa mtindo wa usisimukaji.

• **Seyyed Mohammad Musavi & Mahoor Institute (Iran)**

Muasisi na mkurugenzi wa *Mahoor Institute of Culture and Arts*, ambaye ametoa mchango wa awali katika ukuaji wa muziki na elimu ya muziki wa Iran.

• **Zulkifli & Bur'am (Aceh, Indonesia)**

Wafufuaji wa mapokeo ya nyimbo za *Aceh* ambao wamesaidia uimarishaji wa jamii kwa vijana kupitia ushiriki wao katika Bur'am, kikundi cha nyimbo na ngoma za asili kilichoanzishwa na Zulkifli.

Aidha, Jopo la Majaji wa Tuzo za Muziki za Aga Khan lilimtangaza **Musallam al-Kathiry** kuwa mshindi wa tuzo maalum ya Umahiri katika Huduma ya Urithi wa Muziki wa Omani. Ndugu al-Kathiry, ambaye ni mtafiti wa muziki, meneja wa sanaa, msanii na mtunzi kutoka Muscat, Falme za Oman, ametoa mchango muhimu katika ukusanyaji, uwekaji kumbukumbu, uhifadhi na usambazaji wa muziki wa Omani.

***Wasifu kamili wa washindi wa tuzo unapatikana hapa***

AGA KHAN MUSIC AWARDS

**Jopo la Majaji** lililochagua washindi linajumuisha wataalamu sita wa sanaa wanaoheshimika kutoka Azerbaijan, Bahrain, India, Uturuki, Tunisia na Marekani: H.E. Shaikha Hala Bint Mohammed Al Khalifa, Franghiz Ali-Zadeh, Divya Bhatia, Rachel Cooper, Yurdal Tokcan and Dhafer Youssef.

***Wasifu kamili wa wajumbe wa Jopo la Majaji unapatikana hapa***

Tuzo za Muziki za Aga Khan (AKMA) – ambazo zinatolewa na Programu ya Muziki ya Aga Khan (AKMP), ambao ni mradi wa Taasisi ya Utamaduni ya Aga Khan (AKTC) – zinasimamiwa na **Kamati Kuu** yenye wenyeviti wenza **Mtukufu Aga Khan** na kaka yake, **Prince Amyn Aga Khan**. Wajumbe wengine wa Kamati Kuu ni: **Ara Guzelimian**, Mshauri Maalum, Profesa Mstaafu, *The Juilliard School*, na Mkurugenzi Mtendaji na Mkurugenzi wa Sanaa, Tamasha la Muziki la Ojai (OMF); **Salima Hashmi**, Profesa Mstaafu, Chuo Kikuu cha Taifa cha Beaconhouse (BNU); **Shamsh Kassim-Lakha**, Mwenyekiti ya Bodi ya Wadhamini, Chuo Kikuu cha Asia ya Kati (UCA); **Joseph Melillo**, Mtayarishaji Mtendaji, Mstaafu, Chuo cha Muziki cha Brooklyn (BAM); **Sir Jonathan Mills**, Mkurugenzi, Kongamano la Kimataifa la Utamaduni la Edinburgh (EICS); na **Zeyba Rahman,** Mkurugenzi wa Programu ya Building Bridges katika Taasisi ya *Doris Duke Foundation for Islamic Art*.

***Wasifu kamili wa wajumbe wa Kamati Kuu unapatikana hapa***

Kwa mawasiliano ya habari:
akma@akdn.org
semin.abdulla@akdn.org

**Official hashtags:**#AKMA2022 #AgaKhanMusic #AgaKhanMusicAwards #AKMA #AgaKhanTrustForCulture #AKDN